

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OR-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA**

Simu: +255755967336 / +255757736401
Barua pepe: ipindasecondary98@gmail.com



S.L.P 336
KYELA

KUMB. NA. IPSS/ED/2021/001

SHULE YA SEKONDARI IPINDA

TAREHE 05/12/2020

NDUGU: MZAZI/MLEZI WA.....

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IPINDA.

1. UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao.....amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari IPINDA kuanza kidato cha kwanza mwaka 2021. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021.

2. MAHALI ILIPO.

Shule ya Sekondari IPINDA ni ya Serikali naya kutwa. Ipo Mkoa wa Mbeya Wilaya ya Kyela Kata ya Ipinda, Kijiji cha IPINDA umbali wa KM 3 kutoka Mji wa Ipinda. Shule ipo katika Mazingira mazuri kwa kusomea.

3. MAHITAJI YA SHULE.

Mwanafunzi anatakiwa kuleta vitu vifuatavyo.

3.1. WAVULANA (SARE)

- Suluali mbili, moja rangi ya khaki na nyingine rangi nyeusi.
- Shati mbili zote nyeupe mikono mifupi (tetroni)
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu jozi mbili (2)
- Soksi nyeupe jozi mbili (2)
- T-shirt rangi ya njano.
- Sweta ya rangi ya blue

3.2. WASICHANA (SARE)

- Suruari mbili. moja khaki na nyingine nyeusi
- Visoro 2 rangi nyeupe urefu wa mkono wake.
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu jozi mbili (2)
- Soksi nyeupe jozi mbili (2)
- Sweta ya rangi ya blue
- T-shirt rangi ya njano.

- Hijabu rangi nyeupe kwa wanafunzi wa kiislamu.

4. VIFAA VYA MICHEZO.

4.1. WAVULANA.

- Aje na bukta rangi blue na T-shirt rangi ya njano
- Aje na raba jozi moja na soksi ndefu jozi moja

4.2. WASICHANA.

- Aje na bukta rangi bluei na T-shirt rangi ya njano.
- Aje na raba jozi moja na soksi ndefu jozi moja.

5. VIFAA VYA MASOMO (TAALUMA)

Unatakiwa kuleta vifaa vya masomo kama ifuatavyo.

- Madaftari ya kutosha masomo yote 11 yawe kaunta book Quire 2, au Quire 3, au Quire 4 na aina nyingine za madaftari.
- Kalamu za wino za rangi ya blue au nyeusi.
- Kalamu za risasi na rula na mkebe wa Hisabati
- Begi nadhifu la kubebea daftari na siyo Rambo au foronya.
- Rimu 1
- Kamusi ya Kiingereza kwa Kiingereza aina ya “CONCISE ENGLISH DICTIONARY- OXFORD”

6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Elimu ya Juu, Teknologia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu Nchini na Ofisi ya Raisi TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora yenye majukumu ya Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- i) Kutunza mali za umma.

6.1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile bangi, pombe, cocaine, mirungi, kubeli, mandrax, heroin nakadhalika
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau bendera ya Taifa
- h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
- i) Kuoia au kuolewa
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Kuwa na simu ya mkononi

7. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni. (Fomu imeambatanishwa)
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai (Fomu imeambatanishwa)
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule. (Fomu imeambatanishwa)

8. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KARIBU SANA KATIKA SHULE HII YA IPINDA

.....

RAMADHAN SALUM SIMTENDA

MKUU WA SHULE